https://dspace.org/

# Changamoto Zinazokabili Umiliki na Matumizi ya Ardhi Barani Afrika: Udurusu wa Riwaya Tatu za Karne ya 21

**Muhia, Arthur K.; Mwamzandi, Issa Y.**

**2022**
Mwanga wa Lugha, 7(1), 77-88.
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/775
Muhia, A. K., & Mwamzandi, I. Y. (2022). Changamoto Zinazokabili Umiliki na Matumizi ya Ardhi Barani Afrika: Udurusu wa Riwaya Tatu za Karne ya 21. Mwanga wa Lugha, 7(1), 77-88.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

# Changamoto Zinazokabili Umiliki na Matumizi ya Ardhi Barani Afrika: Udurusu wa Riwaya Tatu za Karne ya 21

*Arthur K. Muhia*[1] *na Issa Y. Mwamzandi*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Nairobi*
[2]*Chuo Kikuu cha Kabianga*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachanganua suala la changamoto zinazokabili umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika kama lilivyosawiriwa katika riwaya za karne ya ishirini na moja, kwa kurejelea riwaya za Chozi la Heri (2014), Msimu wa Vipepeo (2009) na Nakuruto (2006). Ardhi ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika maisha ya binadamu hasa katika uzalishaji mali. Huwa chanzo cha mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na makaazi. Aidha, uwezo wa kumiliki ardhi huwa ni sifa kuu ya maendeleo na mabadiliko mengi katika jamii ambayo yamewahi kushuhudiwa duniani. Tungo za kifasihi tulizoziteua kimakusudi zilifanikisha utafiti huu kwa sababu fasihi huwa imefungamanishwa kibunifu na maisha halisi ya binadamu. Sifa kuu ya riwaya hizi ni kwamba zimeliangazia suala la ardhi kwa mapana. Isitoshe, zimetungwa katika kipindi cha karne ya ishirini na moja ambacho utandawazi umeenea na kuimarika barani Afrika. Ili kufanikisha udurusu huu, tuliligawa suala letu la utafiti katika sehemu tatu kuu: kipindi cha kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na kipindi cha utandawazi. Uchanganuzi matini huu wa kimaktaba uliongozwa na nadharia ya Baada-ukoloni. Umuhimu wa makala haya unatarajiwa kuwa pamoja na kudhihirisha mitazamo ya watunzi mbalimbali kuhusu changamoto katika umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika; pamoja na mapendekezo ya namna za kuzitatua. Tunatarajia kutoa mchango wa kitaaluma kuhusiana na suala hili hivyo kuwafaa watafiti wa baadaye na watunga sera zinazohusiana na suala la umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika.**

**Maneno Muhimu**: Ardhi, Utandawazi.

**Utangulizi**

Makala haya yanahusu uchanganuzi wa suala la changamoto zinazokabili umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika kwa mujibu wa riwaya tatu za karne ya ishirini na moja; *Chozi la Heri* (2014), *Msimu wa Vipepeo* (2009) na *Nakuruto* (2006). Tungo hizi za kifasihi zimefanikisha utafiti huu kwa sababu fasihi huwa imefungamanishwa kibunifu na maisha halisi ya binadamu (Habib, 2011). Riwaya hizi zina sifa kuu ya kuwa zimetungwa katika kipindi cha karne ya ishirini na moja ambacho utandawazi umeenea na kuimarika barani Afrika. Uchanganuzi matini huu wa kimaktaba uliongozwa na nadharia ya Baada-ukoloni.

Ardhi ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika maisha ya binadamu hasa katika uzalishaji mali. Huwa chanzo cha mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na makaazi. Aidha, uwezo wa kumiliki ardhi huwa ni sifa kuu ya maendeleo na mabadiliko katika jamii. Kobia na Njeru (2019) wanayaunga mkono mawazo haya wanaposema kuwa; maendeleo mengi yaliyowahi kushuhudiwa duniani, yanahusiana kwa namna moja ama nyingine na suala la umiliki na matumizi ya ardhi. Wanaendelea kufafanua kwamba suala hili ndilo linalotawala siasa na uchumi barani Afrika.

Utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali zikiwemo biashara, uchumi, siasa na utamaduni. Uhusiano huu unafanikishwa na maendeleo ya teknolojia ya habari yanayoyawezesha mataifa kuwasiliana kwa wepesi (Alomo 2016). Maelezo haya yanaambatana na yale ya Muhia (2019) anayeeleza kuwa utandawazi ni uhusiano wa mataifa ya ulimwengu yaliyoendelea na yanayoendelea katika masuala ya kijamii na kiuchumi unaotiliwa nguvu na mfumuko wa sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Katika makala haya, tulijikita katika

changamoto zinazokabili umiliki na matumizi ya ardhi hasa katika kipindi cha utandawazi kwa mujibu wa riwaya tatu za karne ya ishirini na moja ambazo ni: *Chozi la Heri* (2004) *Msimu wa Vipepeo* (2009) na *Nakuruto* (2006).

Uchanganuzi huu unaongozwa na kudhibitiwa na nadharia ya Baada-ukoloni. Habib (2005) na Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa nadharia ya Baada-ukoloni huchunguza uhusiano uliopo baina ya nchi tawala na nchi zilizotawaliwa ili kuhakiki historia ya utawala wa kikoloni kwa mtazamo wa waliotawaliwa. Hili hufanikishwa kwa kuchunguza athari za ukoloni kwa nchi zilizotawaliwa. Athari hizi hudhihirika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Uchunguzi huo hutarajiwa kuibua mbinu mwafaka za kufanikisha mchakato wa kutatua changamoto zilizopo. Ni katika msingi wa nadharia hii ambapo katika makala haya tunadai kuwa Mwafrika yumo katika harakati za kukabili changamoto zinazokumba umiliki na matumizi ya ardhi hasa kutokana na utandawazi kwa msingi wa riwaya ya Kiswahili.

Mihimili ya nadharia ya Baada-ukoloni ambayo imepewa umuhimu hapa ni pamoja na: Mwafrika kusawiriwa akiwa kiumbe dhaifu asiye na uwezo wa kuchagua alitakalo maishani na asilolitaka, Mwafrika amelazimika kujidunisha na kujichukia kiasi cha kutamani asiwe Mwafrika bali awe mwenye asili ya wakoloni.

**Umiliki na Matumizi ya Ardhi Kipindi cha Kabla ya Ukoloni**

Kihistoria, umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika lilikuwa suala la jamii nzima kinyume na hali ya sasa ambapo huwa suala la kibinafsi. Hili ni kwa mujibu wa riwaya ya *Chozi la Heri* kwenye dondoo ifuatayo:

> “Kabla ya miaka ya hamsini, umiliki wa kibinafsi wa ardhi haukusisitizwa katika jamii yetu. Ilipotokea kwamba kulikuwa na upungufu wa ardhi katika eneo fulani, watu wangehama na kuishi na watu wa ukoo mwingine. Lilikuwa jambo la kawaida kuwapata watu wakiishi na kulima katika mashamba ya majirani, marafiki na jamaa. Baada ya kuyalima mashamba haya kwa muda, yaliishia kuwa yao. Hawakuhitajika kuyanunua kama mnavyofanya sasa.” (*Chozi la Heri,* uk. 9)

Kipindi cha kabla ya ukoloni, umiliki wa ardhi kwa matumizi ya kikulima na makao ulijengwa katika msingi wa wanajamii kushirikiana. Ushirikiano huo ulileta usawa katika umiliki wa ardhi kama nyenzo kuu ya uzalishaji mali. Hili lilihakikisha kuwa kila mwanajamii anaweza kupata mahitaji yake ya kimsingi (Muhia 2019, Makumba 2007, Nangoli 2002 na Mbiti 1989).

Kupitia kwa ukulima na ufugaji, ardhi ndio ilikuwa nyenzo kuu ya kumwezesha Mwafrika kukidhi mahitaji yake ya kila siku. Aidha, biashara ilishamiri kupitia ubadilishanaji wa bidhaa zilizotokana na matumizi chanya ya ardhi. Isitoshe, mifugo iliwafaa wanajamii kwenye shughuli za kiuchumi na hata kijamii kama vile kuwa sehemu ya ulipaji mahari na utoaji kafara. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Nakuruto*. Kabla ya uzalishaji kuingiliwa na ukoloni, ukulima na ufugaji ulizalisha chakula cha kutosha. Mhusika Nakuruto anawakumbusha wanakijiji cha Walatimbi kwamba zamani kabla ya ukoloni, walikuwa wenye mafanikio makubwa. Anaeleza kuwa:

> “Watoto wao walikuwa wakishiba maziwa kiasi cha kuteuka ovyo, mifugo walikuwa wengi kiasi cha kuhitajika kupanua maboma ya kuwasitiri, vijana walijaa misuli na watu walikula na kusaza kutokana na uzalishaji wa vyakula vya kiasili kama mawele, mtama, maboga na mayungwa.” (*Nakuruto*, uk. 114)

Uzalishaji wa zamani ambao haukufuata kasumba za kikoloni uliwahakikishia Walatimbi kuwa na chakula cha kutosha pamoja na mifugo wao. Hali hii pia ilichangia katika kuhakikisha kuwa vijana wa jamii hiyo wana afya ili waiendeleze jamii siku za usoni.

Kabla ya ukoloni, wanajamii walihimiza utunzaji na uhifadhi wa mazingira kutokana na umuhimu wa mazingira asilia katika utengenezaji wa dawa zinazotumiwa kutibu maradhi mbalimbali katika jamii kama anavyodhihirisha mhusika Mzee Kitali katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*. Mzee Kitali anasimulia jinsi mazingira asili yalivyowafaidi wanajamii kupata huduma za matibabu. Masimulizi

yake ni kupitia mdokezo wa maswali kwa mhusika Julia ambaye alikuwa anaitilia shaka nafasi ya mazingira katika matibabu. Mzee Kitali anamuuliza Julia hivi:

> "Wewe hapo ulipo ulifanya nini kila uliposumbuliwa na maradhi ya tumbo? Je, ulipochubuka ukicheza; ulipojikata ukiwa shuleni na hata kuwa na vidonda hatukutumia maji ya msubiri? Je, babangu mwenyewe aliposumbuliwa na shinikizo la damu na hata kuvimbiwa hakutumia majani ya mdalasini? Je, mamako alipokuwa mjamzito hakula terere na managu kuimarisha damu yake?" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 62)

Ndumi, binti ya Julia waliyeandamana naye, anaonekana kuchangamkia ujuzi ulio kwenye maswali ya babu yake, Mzee Kitali. Msimulizi anasema kuwa Ndumi alielekea kuvutiwa na sayansi hii kali ya jadi. Kuvutiwa huku ni jazanda ya nafasi ya mazingira kimatibabu kipindi cha kabla ya ukoloni.

**Umiliki na Matumizi ya Ardhi Kipindi cha Ukoloni**

Mwirabua (2014) anaaeleza kuwa ukoloni hujitokeza pale ambapo nchi tawala hutumia nguvu kupindukia ili kutawala watu ndani na nje ya himaya zao. Utawala kama huo sio tu wa kisiasa bali hata wa kiuchumi na kiutamaduni. Nchi tawaliwa hulazimishwa kutumia mbinu za kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na hata lugha za nchi tawala hivyo kugeuzwa watumwa (Wa Thiong'o, 1993). Katika kipindi cha ukoloni, mkoloni alikiuka haki za Mwafrika za umiliki na matumizi ya ardhi kupitia unyakuzi na ubaguzi katika ugawaji. Mwafrika akageuzwa kuwa masikini na mtumwa katika ardhi yake kama inavyodhihirika kupitia dondoo ifuatayo:

> "Hatua ya mkoloni ya kupuuza sera za Mwafrika za umiliki wa ardhi, na kuamua kujumuisha pomaja ardhi iliyomilikiwa na mtu binafsi, na kuidhinisha umiliki huu kwa hatimiliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii. Katika sera ya kijadi ya umiliki na matumizi ya ardhi, raia wote, hata wageni, walikaribishwa na kugawiwa mashamba, hivyo kupata mbinu za kuyaendesha maisha. Sera mpya ya umilikaji nafsi wa ardhi ilimaanisha kwamba wale walikosa pesa za kununulia mashamba wangekosa mahali pa kuishi. (*Chozi la Heri*, uk. 9)

Sera mpya inayoelezwa kwenye dondoo hii ni kanuni mpya za kikoloni ambazo ziliwakandamiza wale ambao hawakuwa na uwezo wa kununua ardhi. Hali hiyo inafafanuliwa zaidi sauti kwenye fikra za mhusika mkuu, Ridhaa, zinazoweka wazi ubaguzi wa kikoloni kuhusu umiliki na matumizi ya ardhi.

> "Mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sharia ya mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikaji wa ardhi na Waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa…yote yakapata wenyeji wageni…Waafrika…walilazimika kuwa ama vibarua katika mashamba yaliyokuwa yao, au maskwota ambao maisha yao yalitegemea utashi wa Mzungu. Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadowadogo, maskini, wasio na ardhi…jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambao Wazungu wangeamua kuchukua vibarua kupalilia mazao yao." (*Chozi la Heri*, uk. 7)

Sauti hii kwenye fikra za Ridhaa ni uzungumzaji nafsi unaolenga kueleza changamoto walizopitia Waafrika kipindi cha ukoloni. Ardhi ilitwaliwa na wakoloni huku Waafrika wakisalia kuwa maskwota na vibarua hali iliyochangia wao kuwa maskini.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Nakuruto* inasawiri kejeli ya wanaume wanaofanya kazi ya sulubu ili kufanikisha uzalishaji wa kikoloni katika shamba la pamba lilomilikiwa na mlowezi wa kigeni, Bw Brook. Wanaume hawa wanasawiriwa kuwa wenye dhiki kubwa kwa kushindwa kuzikimu familia zao kwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Pamba wanayozalisha, Bw Brook anaisafirisha ughaibuni. Kejeli hii ya kiukombozi inajitokeza wazi zaidi msimulizi anaposema kuwa:

> "Nakuruto alipokuwa akitazama utekelezaji wa kadhia mbalimbali katika shamba hilo, alimwona mwanamume mmoja akipita mbio huku akilalama. 'Nimechoka…Nimechoka kabisa!'…tangu asubuhi sijatia chochote tumboni. Wanangu…hawana lishe, hata mbavu

> unaweza kuhesabu. Mke wangu…kabakia ng'onda utadhani namyima chakula. Chakula kitoke wapi…?...mie mke wangu ametoroka. Kahamia kwao…kisa na maana, simlishi wala simvishi. Sikuwa na wasaa hata wa kuzaa watoto naye kwani kutwa kucha nimo shambani kwa Brook nikimtumikia" (*Nakuruto*, kur. 39-43)

Hapa, Mwafrika anadhihirisha urazini wa kiukombozi kupitia kutathmini uzalishaji. Hili linabainika kupitia kwa jazanda ya mwanamume anayepita mbio huku akinung'unikia kutumikishwa kwa faida ya wenye nguvu za kiutandawazi, akina Brook, wasiojalia mahitaji yake ya kimsingi. Katika shamba la Brook uzalishaji ni wa mazao biashara tu. Mawazo haya ya kiukombozi yanaungwa mkono na Mutembei (2016) anayesema kuwa ukombozi huanzia kwenye fikra ambazo humwezesha anayejikomboa kujitambua, kufanya uamuzi na hatimaye kujikomboa.

Kihistoria, suala la umiliki na matumizi ya ardhi lilichochea vita vya ukombozi dhidi ya utawala dhalimu wa kikoloni barani Afrika. Vita hivi vilijikita katika utwaaji wa ardhi kutoka kwa wakoloni. Ukombozi huu ulihimiza ujamaa katika umiliki wa mali asilia kama ilivyokuwa kabla ya ukoloni kama anadhihirisha mhusika Nakuruto katika riwaya ya *Nakuruto*. Nakuruto anawahimiza Walatimbi kumfurusha Bw. Brook ili kuikomboa ardhi yao na vyanzo vya maji. Bw. Brook ni mlowezi kutoka ughaibuni aliyebinafsisha mto Milu na sehemu kubwa ya ardhi ya Walatimbi karibu na mto huo. Nakuruto anasema kuwa kwa kumfurusha Bw. Brook, Walatimbi wataukomboa mto Milu. Kupitia kwa ukulima na ufugaji utakaofanikishwa kwa maji ya mto huu, wataweza kuzalisha chakula cha kutosha kuwalisha wanajamii wote kinyume na Bw. Brook anayechukua asilimia kubwa ya mazao ughaibuni na kuwaacha wenyeji wakihangaika kwa upungufu wa chakula. Msimulizi anafafanua mafanikio ya ushauri wa kumfurusha Bw. Brook katika dondoo ifuatayo:

> "Umati ulirejea tena kushangilia kuanguka kwa kitovu cha udhalimu…kubomolewa kwa zile kuta zilizojengwa kando ya mto ili kuwazuia wanakijiji kutumia maji. Aliweza kuona watu wakiteka maji kwa shangwe na vigelegele. Kijiji cha Latimbi kikavuma tena kwa uhai mpya. Mashamba yalilimwa na mimea anuwai kukuzwa. Watu walifuga ng'ombe, mbuzi, kondoo na chochote kile kilichoweza kufugwa…mto Milu ukavuma kwa wingi wa maji ambayo awali yalifujwa na dhalimu yule… Haya yalimridhisha Nakuruto hasa alipoona uhai ukichipuka tena katika ardhi iliyokuwa imeharamishwa. Kwa kadri miti ilivyochipua uhai, ndivyo watu walivyochipuza kizazi kilichokita mizizi katika uasili wa mazingira yao." (*Nakuruto,* kur. 50-51)

Dondoo hii inafafanua mafanikio wanayoyapata Walatimbi kutokana na kuhakikisha kuwepo kwa ujamaa katika umiliki wa mali asili kama vile mto Milu. Huu ni ufumbaji wa kijazanda unaokusudia kusawiri hali ya umiliki na matumizi ya ardhi baada ya anguko la ukoloni hivyo umiliki wa mali asilia unakuwa mikononi mwa Waafrika wenyewe.

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* haijabaki nyuma katika hili la kuhimiza ukombozi dhidi ya ukoloni kupitia kutathmini uzalishaji. Hili linadhihirika kwenye dondoo ifuatayo:

> "…sisi hapa tulipo ni maskwota tu. Tunaruhusiwa kulima huo mpunga na kwa kweli unazaa vizuri…mtu anavuna magunia arubaini ya mchele; mwenyewe anaruhusiwa kuuza magunia manne tu!" (*Msimu wa Vipepeo*, kur. 16-17)

Hapa Mwafrika anaonekana mwenye bidii katika uzalishaji unaofuata mkumbo wa kikoloni tu. Kutokana na hali ya kuwa skwota, anayeruhusiwa kumiliki kipande kidogo tu cha ardhi, hana nafasi ya kufaidi kwa asilimia kubwa kutokana na kilimo anachokiendeleza kwa bidii. Anazingatia zaidi kilimo biashara kisichomfaidi kama kinavyowafaidi walowezi kutoka ughaibuni ambao ndio wanaomiliki sehemu kubwa ya ardhi. Walowezi hawa wanamtumikisha Mwafrika kwenye ardhi yake. Dondoo hii imejengwa katika kejeli ya kiukombozi inayomhimiza Mwafrika atathmini mchakato mzima wa uzalishaji kwenye mazingira yake.

**Umiliki na Matumizi ya Ardhi Barani Afrika Kipindi cha Utandawazi**

Utandawazi katika utafiti huu ni sehemu ya ukoloni mamboleo; dhana inayotumiwa na wahakiki wanaojitokeza baada ya enzi ya ukoloni mkongwe kwa maana ya nchi zilizostawi kuingilia masuala

ya nchi zinazoendelea kwa nia ya kuzitawala kisiasa, kiuchumi na hata kitamaduni. Katika ukoloni mamboleo miundo ya kiuchumi kama vile mifumo ya kibiashara ya kibepari na kampuni za biashara za kigeni zinaendelea kukandamiza nchi zinazoendelea na kunyakua rasilimali za mataifa haya yanayoendelea (Mwirabua, 2014). Utandawazi umekuwa kiini cha matatizo katika nchi zinzoendelea barani Afrika kuliko manufaa yake. Miongoni mwa matatizo haya ni janga la kuporwa kwa rasilimali za uzalishaji mali za nchi hizi ikiwemo ardhi. Utandawazi unahimiza kuwepo kwa kanuni za kiuchumi zinazokuza ubinafsi wa kibepari katika harakati za uzalishaji mali. Hili linachangia kuibuka kwa matabaka katika umiliki wa nyenzo za kuzalisha mali kama vile ardhi. Matabaka haya yanagawika katika vikundi viwili vikuu ambavyo huwa na migororo isiyokoma baina yavyo; kundi la matajiri na la masikini (Moyo 2009 na Wa Thiong'o 2009).

**Utandawazi na Kanuni za Uzalishaji Kwenye Kilimo**

Japokuwa utandawazi ni miongoni mwa mabadiliko ya kilimwengu kwa mujibu wa nchi za Ulaya zilizoendelea, Mwafrika amekandamizwa kwa kufuata mkumbo tu wa wenye kueneza utandawazi hata kwenye masuala yanayotarajiwa kumwezesha kukidhi mahitaji yake ya chakula cha kila siku kama vile ukulima na ufugaji. Hali hii inaelezwa na mhusika Tila katika riwaya ya *Chozi la Heri* pindi tu baada kutoka shuleni ambako mwalimu Meli aliongoza mjadala wa kina kuhusu mifumo ya uzalishaji mali barani Afrika ili ilivyobadilika, kuanzia wakati wa ujima, ukabaila, ubwanyenye, ujamaa hadi sasa jamii yao inapopambana na utandawazi. Mjadala huu ulikuwa unaangazia mafanikio ya baada ya uhuru, yaani baada ya anguko la ukoloni mkongwe:

> "Je, miaka hamsini ya uhuru imetukuza kiuchumi au tumebaki kuwa wategemezi wa hao hao ambao walitupa uhuru? Hatuna tunalolimiliki. Wageni ndio wanaoamua wakuze nini katika ardhi yetu! Tunabaki kuwategemea, si kwa lishe tu, bali pia kwa ajira…hata kidogo tunachokikuza chaenda kumfaidi huyo huyo aliyetupa uhuru. Sijui kwa nini hatujaweza kuijisagia kahawa au chai yetu. Itakuwaje mbegu ziwe zetu, tuchanike kulikuza zao lenyewe, kisha tumpelekee mwingine kwenye viwanda vyake, alisage na kutuuzia hiyo hiyo kahawa na chai kwa bei ya kukatisha tama…Fikiria wewe, mtu aje kutoka huko, anyakue ardhi, alime, afuge, kisha miaka hamsini baada ya kifo chake, bado anakuuzia maziwa yaliyoganda kutoka huko ahera aliko!" (*Chozi la Heri*,kur.5-6)

Maelezo haya ya mhusika Tila katika mjadala wake na babake, Ridhaa, yanaishia kwa kuwarejelea Wafrika kijazanda kama watoto wa miaka hamsini ambaye hajasota wala kusimama dede. Jazanda hii inafafanua namna Mwafrika amesalia kuwa mtegemezi wa wakoloni waliomtawala. Isitoshe, ni ithibati kuwa mfumo wa elimu kwenye jamii hii unaliangazia suala la utandawazi kama changamoto hasa katika umiliki na matumizi ya rasilimali ikiwemo ardhi.

Tamaa ya kuusaka utandawazi inawafanya Waafrika waliokuwa wakilima ili kukidhi mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula, watenge ardhi kubwa ili kukuza mazao yaliyoweza kuvutia masoko ya kimataifa. Hii ni kasumba ya kiutandawazi ambayo haijali maslahi ya kimsingi ya waliozalisha kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Nakuruto* kupitia kwa dondoo ifuatayo:

> "Wanavijiji wengine waliacha kabisa kukuza vyakula vyao vya kiasili ati kwa sababu upepo huo hautavuma upande wao. Mashamba yakakuzwa mimea kutoka ughaibuni iliyoambiwa kuwa itawapa fursa ya kunusa harufu ya nta. Hata samadi pia zilitoka huko ughaibuni kwani zile za kiasili ziliambiwa zinafukuza harufu hiyo nzuri ya nta. Udongo nao ukatoholewa ili uzalishe mazao ya ughaibuni. Wanavijiji waliacha kukuza mimea iliyohimili mazingira ya asili yao na kukuza ile isiyokubali mazingira hayo. Walifahamishwa na akina Quick Buck kwamba wakifanya hivyo, upepo wa harufu ya nta utabadilisha mkondo na kuvuma upande wao…nao mifugo waliozoea mazingira yao walitoweka. Badala yake, wale wa kutoka ughaibuni ndio waliofugwa ili wawezeshe kunasa harufu ya nta…chochote kilichoweza kusaidia kuinasa harufu hiyo kilikubaliwa upesi bila tafakuri" (*Nakuruto* kur. 101- 102)

Dondo hii inasawiri hali ambapo Mwafrika amekosa kujithamini hivi kwamba hakosi tu kupanda mimea asilia na kufuga mifugo asilia jambo litakalomwezesha kuzalisha chakula, bali pia hana imani na mbolea asilia kutokana na kasumba za kiutandawazi. Mbinu za kiasili za uzalishaji ambazo

zilijumuisha ufugaji wa wanyama na upanzi wa miti kama njia ya kuongeza rutuba zinapuuzwa. Badala yake, Mwafrika anakimbilia utohozi wa udongo kwa kutumia kemikali zinazoathiri uwezo wa mchanga kuhimili rutuba. Waafrika hawajali hata kufanya utafiti kuhusu kemikali hizi. Maadamu wameambiwa zitawafanya wafaidi utandawazi, wao wanafuata tu.

Kupitia kwa mhusika Mzee Saluda, riwaya hii ya *Nakuruto* inaendelea kuifafanua hali hii. Wanaoendeleza changamoto za umiliki na matumizi ya ardhi kupitia kwa utandawazi wanafuga mifugo wengi na mwishowe bidhaa kusafirishwa ughaibuni na kuwaacha Waafrika wakitaabika. Hali hii sio tofauti katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* kama inavyodhihirika kupitia kwa maelezo yafuatayo ya mhusika Mzee Kitali:

> "…sisi hapa tulipo ni maskwota tu. Tunaruhusiwa kulima huo mpunga na kwa kweli unazaa vizuri…mtu anavuna magunia arubaini ya mchele; mwenyewe anaruhusiwa kuuza magunia manne tu! Mengine mali ya serikali! Hamna anayejali kama una jamaa; unaumwa; una ardhi…una nini! Shauri yako na maisha yako! Sasa raha iko wapi kama mavuno wanafaidi hao wanaoishi huko Kitambasie; wamejitambaza tu kwenye penu za ofisi zao kubwa kama mijusi, wasijue hata hiyo sura ya mpunga! (*Msimu wa Vipepeo*, kur. 16-17)

Mzee Kitali analalamikia kilimo chenye kulenga soko la ughaibuni ambalo limeelezwa kijazanda kama mji wa Kitambasie kwenye dondoo, pasipo kujali maslahi ya mkulima. Wanaofaidi kilimo cha mpunga huko ughaibuni hawajishughulishi na ukulima wenyewe. Hali hii inamfanya Mzee Kitali kuhisi kuwa uhuru alioupata Mwafrika baada ya anguko la ukoloni mkongwe ni wa kidhahania tu. Aidha, anamfafanulia Kanda kuhusu hali hii kupitia kwa ufumbaji wa kijazanda unaoulinganisha uhuru huo na maji yaliyomwagika na kukauka kabla ya kumfikia mwenye kiu (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 17).

Utandawazi pia umewafanya Waafrika kupanda mimea ya ughaibuni na kufuga mifugo waliotoka ughaibuni. Hili ni mojawapo wa athari hasi za uigaji wa mambo yasiyokuwa na uasili wa maisha ya Waafrika. Tukirejelea riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, tunakumbana na kijiji ambacho kihistoria kilikuwepo kizazi kilichowahi kuishi katika eneo hilo ambacho kilifurikwa na utajiri kiasi kwamba maziwa ya ng'ombe yalitumiwa kunawia mikono lakini sasa wenyeji ni maskini. Umaskini wao umetokana na kuvurugika kwa ukulima wa miwa na makadamia baada ya kufilisika kwa kiwanda cha sukari na kingine cha njugu za makadamia kutokana na usimamizi mbaya wa wabunge wa eneo hili waliomtangulia Mkurutu. Badala ya Mkurutu kufufua viwanda hivi ili kuwezesha ukulima kunawiri, anachukua pesa za wizara zilizotengewa wagonjwa wa ukimwi na kuanzisha mradi wa kufuga vipepeo (Papilio Butterfly Centre) akilenga soko la kitandawazi kama inavyodhihirika kwenye dondoo ifuatayo:

> "Huyu ni mwekezaji…si mnajua tunaishi katika ulimwengu wa…utandawazi…mfumo unaolenga kuhakikisha kuwa faida za kiuchumi hazibakii kwenye mataifa fulani ya Ulaya na Marekani tu…baadaye walielezewa kuwa mradi huu ulikuwa na matokeo mazuri kwa wenyeji wa eneo bunge hili. Kwamba palikuwa na soko zuri la kuuza hizo 'pupae' huko Uingereza, Ufaransa, Marekani na Ujerumani ambako hutiwa kwenye 'green houses' ili wenyeji wa huko wakawatazame vipepeo." (*Msimu wa Vipepeo*, kur. 205-207)

Mradi huu hauzingatii namna za ukulima na ufugaji kabla ya ukoloni na utandawazi ambazo ziliibua utajiri katika kizazi kilichotangulia. Hauzalishi chakula wala kuwaletea Waafrika faida yoyote kwani hatimaye unakosa kufanikiwa. Haya yote ya uzalishaji unaofuata mkumbo tu yanafanywa ili kuukaribisha utandawazi pasipo kutafakari athari zake hasi.

Kilimo cha mazao biashara kinapunguza kilimo cha mazao chakula na kusababisha njaa. Kwa mfano katika riwaya ya *Nakuruto*, kuwepo kwa kiwanda cha pamba kunawafanya wanavijiji kutupilia mbali kilimo cha chakula kwa tamaa ya kushiriki biashara ya kiutandawazi kama inavyodhihirika kwenye dondoo ifuatayo:

> "Mashamba ya vijijini yaliacha kulimwa, watu wakakimbilia mashamba makubwa makubwa yenye kuzalisha mazao ya kusafirishwa nje ya vijiji. Konde za watu zikamea magugu kwa

kukosa huduma. Hata wale waliokuwa wakilima ili kukidhi mahitaji yao walitenga ardhi kubwa ya vikataa vyao kukuza mazao yaliyowezesha kutega harufu ya nta." (*Nakuruto*, uk.140)

Katika dondoo hii, harufu ya nta ni ufumbaji wa kijazanda unaorejelea kasumba za kiutandawazi zilizowafanya wanakijiji kutelekeza uzalishaji wa mazao yaliyowasaidia kukidhi mahitaji yao ya chakula. Jazanda hii inakusudia kuwakejeli wanavijiji ili wapone kutokana na matatizo ya kisaikolojia ya kukosa kujithamini kama unavyopendekeza mhimili wa kwanza wa nadharia ya utafiti huu.

Tukio lingine katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* linalolenga kutathmini uzalishaji kama mkakati wa kiukombozi linahusu kufeli kwa mradi wa kiutandawazi wa kufuga vipepeo. Raia mmoja ambaye alifahamika kijijini kwa tabia yake ya kuibeba redio yake ndogo aliyoifumia mfukoni na kudai hataki kuachwa nyuma na ulimwengu, anamkejeli waziri Mkurutu na mradi wake wa vipepeo. Raia huyu anasema kuwa ule ni mradi wa utandawizi badala ya utandawazi. Hii ni kejeli ya kiukombozi ambayo inadokeza hali ya Mwafrika kutofaidi mradi huu kama inavyodhihirika baadaye kwenye dondoo hii:

> "…siku ya kusafirishwa kwa pupa za vipepeo wa watu wa Kisangu…wote wakatamani kuona bidhaa zao zimepakiwa kwenye gari lenyewe na wamewahi mjini…muda mfupi baadaye lori lilianza safari…nyuma wanakijiji waliachwa wakiimba nyimbo za furaha…dakika thelathini baadaye mawingu yaliyokuwa yanatisha kwa mbali yameshakusanyika pamoja na hatimaye kuangusha mvua kubwa ajabu…humo walimokwamia…wenye lori waliishia kukwamuliwa kutokana na msaada wa kampuni yao siku mbili baadaye…walipofungua sehemu ya nyuma ya lori waliachama. Zile pupa zilikuwa zimepasuka na vipepeo wasiokuwa na nguvu kutoka kwenye vimvugu vyao. Wawili watatu walikuwa wakiruka hapa na pale. Huko Kisangu wanakijiji walikuwa bado wakifanya mahesabu yao ya mapato yaliyowasubiri." (*Msimu wa Vipepeo*, kur. 276-279)

Dondoo hii inadhihirisha hali ya kukatisha tamaa kwa wanakijiji waliochangamkia ufugaji wa vipepeo kwa soko la kiutandawazi kwa matumaini ya kupata mapato ya kiwango cha juu. Miradi ya kiutandawazi kama huu isiyotathmini uzalishaji kwa mujibu wa mahitaji ya Mwafrika imesawiriwa ikiwa imefeli kama njia ya kuhimiza ukombozi. Ukombozi ukipatikana Mwafrika atatoka katika hali aliyonayo ya kutamauka.

Kukosa kutathmini uzalishaji kunasababisha uzalishaji wa chakula kuwa wa kiwango cha chini. Hali hii inasababisha Waafrika waathirike na njaa. Hili linawafanya kutegemea chakula cha misaada ambacho wakati mwingine wanapokea misaada yenye sumu kama inavyosawiriwa katika riwaya ya Msimu wa Vipepeo. Msimulizi anasema kuwa:

> "…watu walipewa chakula kilichotolewa na serikali majuzi tu. Waliokula walianza kulalamikia maumivu ya tumbo; wengine macho yao yakabadilika na kuwa ya manjano; matumbo yakavimbiana na hatimaye, kama majani ya mitende…wakaanza kupukutika mmoja baada ya mwingine; kwingine jamaa nzima zimefutwa na mahindi hayo." (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 245)

Magonjwa na vifo kwenye dondoo ni ufumbaji wa kijazanda unaosawiri athari hasi za utegemezi wa misaada. Kama serikali ingekuwa imewawezesha wahusika walioathirika kulima mahindi yao wenyewe, pengine hawangeathirika na njaa kiasi cha kupelekewa mahindi yaliyoharibika.

Misaada ya serikali isipofua dafu, serikali inalazimika kuomba misaada kutoka ughaibuni ambako wanapata misaada ya chakula cha mbwa kutoka ughaibuni ili walishwe Waafrika kana kwamba wao sio binadamu kamili. Hili linasisitizwa kupitia dondoo ifuatayo:

> "Mellisa aliwazia tatizo hili la njaa. Nchi yake imekuwa huru kwa miaka…lakini bado inashindwa kujilisha yenyewe…alikumbuka majuzi serikali ilikuwa ikitoa tangazo kuomba msaada wa chakula kutoka kwa mataifa mengine…akakumbuka jinsi kampuni moja ya kutengeneza chakula cha mbwa huko New Zealand ilivyojitolea kutoa tani kadhaa za chakula hicho kilishwe watoto mayatima waliokumbwa na njaa nchini." (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 246)

Dondoo hii ni kejeli ya kiukombozi inayofafanua athari hasi za kukosa kutathmini uzalishaji. Mwafrika amekumbwa na njaa na akitafuta msaada ughaibuni, anapata misaada ya kumshusha hadhi

kama vile chakula cha mbwa. Mwanahabari mmoja shupavu anamkabili waziri wa afya anayeongoza kamati ya serikali inayohusika na tatizo la njaa kuhusiana na msaada wa chakula cha mbwa kutoka New Zealand ili kuwalisha Waafrika wenye njaa. Anamuuliza waziri maoni yake kuhusu msaada ule. Usemi wa waziri kuhusu msaada huu ni kuwa:

> "…sisi tuko tayari kupokea msaada kutoka kwa yeyote yule…tunaikaribisha misaada ya hao na hata ya wengine." (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 246)

Jibu hili la waziri ni kejeli ambayo inamhimiza Mwafrika kuwania ukombozi ili aepuke kudharauliwa huku. Hili linaungwa mkono na mhimili wa kwanza wa nadharia ya utafiti huu kuwa kazi za sanaa zikusudie kumponya Mwafrika kutokana na matatizo ya kisaikolojia yanayotokana na kudunishwa kwake. Waafrika wakome kuonekana duni kiasi cha kustahili kulishwa chakula sawa na mbwa bali wawezeshwe kuzalisha chakula chao wenyewe.

Uwaniaji wa ukombozi katika uzalishaji wa mazao chakula unazinduliwa na mhusika Mutanu katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*. Baada ya Mutanu kuhitimu masomo ya lishe katika chuo kikuu cha Kitambasie, anaamua kujitolea kwenda na shirika lisilo la kiserikali kuwahudumia wakaazi wa sehemu ya nchi ambayo ilikumbwa na tatizo la ukame kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Mutanu anashangaa kwa nini Waafrika hawajaweza kutatua tatizo kama hili. Mshangao wake unadhihirika kupitia usemi huu:

> "Mama mbona tunashindwa kama nchi kuwa na mipango mizuri ya kupambana na njaa? Kila wakati tunategemea misaada, hata ya chakula! Nchi yetu imeishia kuwa nchi ya bakuli-ehh, nchi ya kushika bakuli kuomba misaada kutoka kwa mataifa mengine" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 246)

Masikitiko haya ya Mutanu yenye kuwakejeli wategemea misaada ni usemi wa kikombozi ambao unafika kileleni anapoeleza kuwa suluhisho la janga hili liko na Waafrika wenyewe. Waafrika wenyewe wazalishe chakula cha kujilisha.

**Utandawazi na Ubinafsishwaji wa Mali Asilia**

Changamoto nyingine ya utandawazi kwa ukulima na ufugaji ni kubinafsishwa kwa mali asilia ambayo awali yalifaa kuwafaidi wanajamii wote pasipo kubagua. Hili linadhihirika katika riwaya ya *Nakuruto* kupitia kwa wenyeji wa eneo la Latimbi. Walatimbi ambao zamani walikuwa wamiliki wa maji ya mto waliozawadiwa na maumbile wanatumikishwa bila huruma na tajiri mmoja wa kiutandawazi anayeitwa Bw. Brook. Tajiri huyu ameyabinafsisha maji ya mto huo ili apande pamba iliyokusudiwa kusafirishwa ughaibuni pasipo kujali kuwa maisha ya watu hawa yalitegemea mto huu (*Nakuruto*, uk. 37).

Mtu mmoja anaubinafsisha mto huku kijiji kizima kikisota bila maji kwa matumizi yao ya nyumbani. Iliwabidi Walatimbi kuyanunua maji kutoka kwa mifereji ya Bw. Brook au kukinga maji ya mvua kwenye paa na viambaza vya vijumba vyao. Baada ya kubinafsisha mto, Bw. Brook anawapokonya Walatimbi ardhi ili kuendeleza kilimo cha pamba. Wanakijiji wanabaki kulihudumia shamba hilo ili wakatiwe vijishamba ambamo walikuza mazao yao duni na juu yake Bw. Brooke akawatoza kodi katika hayo mazao duni kama kanuni ya kiutandawazi ya kukuza na kuimarisha uchumi wa mtu binafsi pasipo kuijali jamii pana.

**Utandawazi na Uharibifu wa Mazingira**

Vilevile utandawazi umechangia katika uharibifu wa mazingira. Kimsingi, mazingira ni maumbile yanayomzunguka binadamu maishani mwake aidha yaliyoumbwa na Muumba kama vile milima, mabonde, mito na kadhalika au yaliyoumbwa na binadamu mwenyewe kama vile utamaduni, mifumo ya kiutawala miongoni mwa mengine. Binadamu ana uwezo wa kuyahifadhi na kuyastawisha mazingira ama kuyaharibu na kuyaangamiza. Katika makala haya , utandawazi unaelekea katika kuyaharibu na kuyaangamiza mazingira ya Mwafrika.

Ayaa (2013) anadai kuwa zamani Waafrika walitegemea tajriba za jamii katika uhifadhi wa misitu na vyanzo vya maji na wakafaulu katika uhifadhi huo. Miongoni mwa tajriba hizi ni imani kuwa

miungu waliishi kwenye mazingira haya ama mazingira yaliyohifadhiwa ndio njia ya kuifikia miungu. Utandawazi unasababisha kupuuzwa kwa tajriba hizi zilizohimiza utunzaji wa misitu na vyanzo vya maji. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Nakuruto* ambapo mhusika Nakuruto anaeleza mandhari ya misitu katika kijiji cha Latimbi kabla na baada ya utandawazi kwa maneno yafuatayo:

> "Kijiji hiki kilikuwa na misitu yenye aina nyingi za miti ya kiasili kama vile mivule, mipingo, mikuyu na mibambakofi...kama mnadhani ninayosema ni uzushi tu, tazameni mto Milu jinsi ulivyokauka kwa sababu ya uharibifu wa miti iliyositiri kingo zake. Mto sasa hauna maji ya kushikilia uhai wenu au hata wa mifugo wenu. Uchafuzi huu wa mazingira umetokana na mbio za walafi miongoni mwenu kutafuta harufu ya nta." (*Nakuruto*, kur. 108-114)

Harufu ya nta katika dondoo hii ni ufumbaji wa kijazanda unaorejelea kasumba za kiutandawazi zinazoendeleza uchafuzi wa mazingira. Imetumika kudhihirisha namna tamaa ya kuusaka utandawazi imesababisha ukataji ovyo wa miti. Hili linasababisha kukauka kwa mto ambao binadamu na mifugo waliutegemea kwa mahitaji yao ya maji.

Riwaya hii ya *Nakuruto* inaendelea kufafanua uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji pamoja na athari zake katika kijiji cha Maweni. Baada ya wanakijiji wa Maweni kuhamishiwa eneo lisilofanikisha ukulima ili kutoa nafasi kwa uchimbaji madini kwa minajili ya soko la kiutandawazi, waliingilia shughuli ya ukataji ovyo wa miti ili wachome makaa waliouza katika vijiji jirani kama njia ya kujikimu maishani. Uchomaji makaa ukasababisha ukame kwa kukosekana kwa mvua. Baada ya ukataji wa miti, waligeukia kuteka mchanga na kuukusanya mafungu wakawauzia wajenzi wa mtaa wenye makasri ya waliowahamisha ili wapate nafasi ya kuchimba madini.

Uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji pia umeangaziwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo wawekezaji wa kigeni kama vile Wataliano waliingilia maeneo ya fukwe za bahari na kujenga makaazi kama inavyodhihirika kwenye dondoo hii:

> "...ni kama wanajenga kisiwa kidogo pale; bustani ndogo ya Wataliano pekee! Ndio utandawazi wenyewe huu!" (*Msimu wa Vipepeo*, uk 217)

Dondoo hii inafanua jinsi maingiliano ya kiutandawazi yameruhusu raia kutoka nchi zilizoendelea kunyakua ardhi na kujenga katika maeneo ya vyanzo vya maji kinyume na matarajio ya Waafrika. Badala ya kujenga kwenye maeneo ya bahari ambayo ni chanzo cha maji, Waafrika walikuwa wakiendeleza shughuli za uvuvi tu katika maeneo haya kabla ya kuingiliwa na utandawazi. Ujenzi katika maeneo haya unaathiri kwa njia hasi shughuli za kiuchumi kama vile uvuvi.

Utandawazi umesawiriwa kuwa changamoto inayoyahujumu mazingira kama vile majengo yenye umuhimu wa kuhifadhi turathi na utamaduni wa Mwafrika. Tukirejelea riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (kur. 46-48), madai haya yanadhihirika kupitia kwa matendo ya wahusika Mkurutu na Fabio. Mkurutu, ambaye ni waziri wa utalii na mazingira, anashirikiana na Fabio, ambaye ni mwanasheria, kumuuzia Mzungu mmoja jengo muhimu kihistoria katika eneo la kisiwa cha Kisiwandeo. Umuhimu mkuu wa jengo hili ni kuwa, lilikuwa linamilikiwa na mshairi maarufu wa zamani. Tajriba na mwonoulimwengu wa mshairi huyu wa zamani ni sehemu ya utamaduni wa Mwafrika. Kwa hivyo, kuhifadhi jengo alimoishi ni sehemu ya utunzaji wa utamaduni huo. Mnunuzi Mzungu hapa ni jazanda inayoakisi soko huria linalopendekezwa na utandawazi. Licha ya umuhimu wa kitamaduni wa jengo hili lililomilikiwa na mshairi maarufu wa zamani katika kisiwa ambacho msimulizi anadai kilikuwa na historia ndefu, linageuzwa kuwa bidhaa inayouzwa sokoni. Mazungumzo baina ya Fabio na Mkurutu kuhusu jengo hili yanatubainishia kuwa maarifa asilia ya Kiafrika yamekuwa tepetevu kwa kuingiliwa na utandawazi kiasi cha kushindwa kuzuia uuzaji wa jengo hili.

Utamaduni wa Mwafrika ulihimiza utunzaji na uhifadhi wa mazingira kutokana na umuhimu wa mazingira asilia katika utengenezaji wa dawa zilizotumiwa kutibu maradhi mbalimbali katika jamii. Madai haya yanaungwa mkono na Ayaa (2013) na Nangoli (2002) ambao wanasema kuwa, matabibu wa kitamaduni waliamini kuwa mimea iliyotumika katika kutengeneza dawa haikufaa kuangamizwa bali kutumiwa kwa uangalifu ili kuhakikisha inaendelea kuwepo. Imani hii inatokana na mawazo kuwa ukiangamiza mmea uliotumiwa kutengeneza dawa, mgonjwa aliyetibiwa kwa kutumia dawa hiyo pia ataangamia. Kwa hivyo walitumia sehemu tu ya mimea husika kwa nia ya kuhakikisha mmea

huo unaendelea kuwepo kwa matumizi ya baadaye. Utaratibu huu umeathirika kutokana na utandawazi kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Nakuruto*. Msimulizi anasema:

> "Nakuruto akaona afya za wanavijiji wengi zikizoroteka kutokana na mahangaiko yale ya kusaka dafina ya Bw. Quick Buck." (*Nakuruto*, uk 140)

Hapa mhusika Nakuruto anasema kuwa afya za wahusika zimezorota kutokana na uharibifu wa mazingira ambayo yalitegemewa kuzalisha dawa za kuimarisha afya. Uharibifu huu umetokana na shughuli za kiutandawazi; zinazolenga kuimarisha ubepari ambazo zimerejelewa kama usakaji wa dafina ya Bw. Quick Buck.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, hali hii ya utandawazi kuathiri utaratibu wa mazingira kuwa sehemu ya matibabu unadhihirika kupitia kwa mhusika Julia ambaye anamgombeza babake, Mzee Kitali, kwa kumwandalia mamake Julia dawa kwa kutumia mimea asilia.

> "Julia aligomba alipomkuta babake, Mzee Kitali akiandaa dawa za kienyeji kwa ajili ya mkewe… Mbona tusimpeleke mama hospitalini badala ya kumpa mizizi hii? Baba huu ni uchawi na ushirikina!" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 62).

Mzee Kitali, analijibu dukuduku hili la Julia ambalo ni kinaya kwa kusimulia jinsi mazingira asilia yalivyowafaidi wanajamii kupata huduma za matibabu kwa maneno yafuatayo:

> "Uchawi? Huko kuishi maisha ya Uzunguni naona kunakuzuzua mwanangu! Wewe hapo ulipo ulifanya nini kila uliposumbuliwa na maradhi ya tumbo? Je, ulipochubuka ukicheza; ulipojikata ukiwa shuleni na hata kuwa na vidonda hatukutumia maji ya mshubiri? Je, babangu mwenyewe aliposumbuliwa na shinikizo la damu na hata kuvimbiwa hakutumia majani ya mdalasini? Je, mamako alipokuwa mjamzito hakula terere na managu kuimarisha damu yake?" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 72)

Maneno haya ya Mzee Kitali yanadhihirisha wazi kuwa utandawazi anaourejelea kama 'kuishi maisha ya Uzunguni' umeathiri kwa namna hasi imani ya Mwafrika kuhusu uwezo wa mazingira asilia katika kuponya maradhi mbalimbali kama inavyodhihirika kwenye dondoo.

**Hitimisho**

Katika makala haya, ilidhihirika kuwa utandawazi ni chanzo cha changamoto nyingi zinazokabili umiliki na matumizi ya ardhi barani Afrika. Changamoto hizi za kiutandawazi zina asili yake kwenye sera za kikoloni. Kwa hivyo utandawazi unaelekea kuwa akisiko la ukoloni. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa hali ya kufuata mkumbo tu wa wenye kueneza utandawazi kwenye ukulima na ufugaji. Mwafrika anapuuza uzalishaji wa mazao asilia ambayo kwa kiasi kikubwa ni mazao- chakula. Badala yake anang'ang'ania kuzalisha mazao yanayoweza kuvutia masoko ya kimataifa ambayo kwa kiasi kikubwa ni mazao-biashara. Riwaya tulizozichanganua zinasisitiza kuwa utamaduni wa Mwafrika unahimiza kutathmini uzalishaji. Hili linafanikishwa kwa kuhimiza kuwepo kwa mimea na mifugo asilia inayohimili mazingira alimo Mwafrika badala ya kukimbilia mifugo na mimea kutoka ughaibuni inayomlazimu kutohoa udongo akitumia kemikali zenye athari hasi kwa ardhi. Kukosa kutathmini uzalishaji kunasababisha uzalishaji wa mazao- chakula kuwa wa kiwango cha chini, kiasi cha kuibuka kwa janga la njaa. Janga hili linamfanya Mwafrika awe mtegemezi wa misaada kutoka ughaibuni.

Changamoto nyingine ya utandawazi inayohusiana na ukulima na ufugaji ni ubinafsishaji wa mali asilia kama vile mito hivyo kuinyima jamii pana nafasi ya kufaidi rasilimali hizi. Riwaya tulizozichanganua zinapendekeza kuwa suluhisho ni kuwepo kwa ujamaa katika umiliki wa mali asilia kama unavyosisitiza utamaduni wa Mwafrika. Hili litahakikisha kuwa mali asilia kama vile ardhi na mito inawafaidi wanajamii wote bila kubaguana.

Uchanganuzi wa riwaya tulizozichagua umedhihirisha kuwa utandawazi una mchango mkubwa katika uharibifu wa mazingira. Hili ni kutokana na kasumba za kiutandawazi kupuuza utamaduni wa Mwafrika unaohimiza utunzaji wa mazingira. Utamaduni huu ni kama vile imani kuwa miungu waliishi kwenye mazingira yaliyohifadhiwa. Matokeo ya upuuzaji huu ni kuibuka kwa majanga kama

vile kuwepo kwa joto jingi kupindukia ulimwenguni na ukame. Ili kuepuka majanga haya, imebainika kuwa Mwafrika hana budi kuzingatia utamaduni unaohusu uhifadhi wa mazingira.

Utandawazi pia umechangia katika kufifia kwa majengo yenye umuhimu wa kuhifadhi turathi na utamaduni wa Mwafrika. Makala haya yanahimiza utunzaji wa majengo yenye umuhimu wa kuhifadhi historia ya jamii kama suala la kimazingira. Majengo haya yakiendelea kuwepo yanaweza kuwa vivutio vya watalii hivyo kumletea Mwafrika kipato.

Kasumba za kiutandawazi zinawafanya Waafrika kudunisha uwezo wa mimea asilia kutumika katika utengenezaji wa dawa zinazotumiwa kutibu maradhi mbalimbali. Badala yake, utandawazi unapendekeza matumizi ya mbinu za kisasa za matibabu zisizozingatia mchango wa mimea asilia. Riwaya nilizozichanganua zinadhihirisha kushindwa kwa mifumo ya matibabu ya kiutandawazi isiyozingatia uwezo wa mimea asilia na kufanikiwa kwa matibabu yanayotumia mimea asilia kama mkakati wa kiukombozi. Isitoshe misaada ya mashine zinazotumika katika matibabu ya kiutandawazi kutoka ughaibuni zinaandamana na utegemezi wa kimaarifa. Zinapokuwa na kasoro, Mwafrika hana uwezo wa kuzirekebisha mwenyewe pasipo msaada kutoka ughaibuni.

**Marejeleo**


Alomo, S, O,. (2016). *Uwakilishi wa utandawazi katika riwaya mpya: Said A. Mohamed na W. K. Wamitila*. Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Ayaa, D, D,. (2013). *Effects of changes in indigenous environmental knowledge systems on the bio-physical environment and community livelihoods in Teso ditrict, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Habib, M. A. R. (2005). *A history of literary criticism from Plato to the present*. Malden: Blackwell Publishing.

Kobia, J, M. & Njeru, M, K., (2019). Usawiri wa mizozo ya ardhi katika riwaya ya kiswahili: Mfano wa riwaya ya *Kufa Kuzikana*. Katika Ponera, A,S., & Badru, Z, A,. (Wahariri), *Koja la taaluma za insia*. (kur. 339-355) Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.

Matei, A. K. (2014). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publisher

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn.

Muhia, A., K. (2019). *Ukombozi wa maarifa asilia ya Kiafrika katika kipindi cha utandawazi: Uchanganuzi wa riwaya tatu za karne ya 21*. Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Kabianga. (Haijachapishwa).

Mutembei, A. (2016) *Dhima ya lugha ya mawasiliano katika jamii: Kiswahili na mkakati wa usomaji kuelekea umajumui wa Kiafrika*. Imerejelewa kutokahttp://journals.udsm.ac.tz

/index.php/kcl/article/viewFile/726/843

Mwirabua, A. (2014). *Ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia teule*. Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Njogu, K. na Chimerah R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi. Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2006). *Msimu wa vipepeo*. Nairobi: Video-Muwa Publishers.

Wa Thiong'o, N (1993). *Moving the Centre*. London: James Currey.